

Swahili transcript:

Nicholaus: Swali lingine ambalo nilikuwa nafikiria ni kwamba, imetokea kwamba, serikali imejenga shule nyingi, na wana jamii, vijiji vimejenga shule nyingi, sasa mwisho wa siku kumekuwa na upungufu wa walimu. Na ikatokea kwamba, sasa hivi kama ukimaliza kidato cha sita, halafu chuoni ukawa hujaingia, unaweza ukachagua kwamba ukafundisha labda mwaka mmoja, miaka miwili. Labda kwamba ,huu mfumo mnavyoangalia, kwamba utatusaidia kukuza elimu ama kuna mikikimikiki, kwa sababu ukiangalia kwamba zipo shule, wanafunzi wapo mashuleni lakini walimu hawapo, na kwamba tatizo la hili ikawa ni kuwachukua hawa vijana ambao wamemaliza na wapo nyumbani kwa muda mfupi kwa kuwatumia. Labda nyie mnafikiria nini kuhusu huu uamuzi mzima wa kufanya hivi?

Mtoa mada: Yaah! mimi kwa upande wangu, swali la walimu wa crush program, katika taifa lolote ili tuweze kufanya maendeleo, lazima tuwekeze katika elimu. Lakini si suala tu la kuwekeza katika elimu, ni tunawekeza katika elimu yenye ubora wa kiwango gani? Sasa, mimi sifikiri hata kidogo kwamba, maana tumekuwa na tatizo moja katika taifa, tumekuwa tukiona kwamba suala la ualimu, taaluma ya kuwa mwalimu, ni taaluma tu ambayo haihitaji uzoefu wa kutosha, haihitaji akili nyingi, haihitaji experience kubwa. Na wakati mwingine imekuwa ikichukuliwa kwamba ni watu ambao wameshindwa maisha, kwamba kwenda kuwa mwalimu ni last alternative (yaah!). Na hii imekuwa ni sababu kubwa ya kwa nini tumekuwa tuko nyuma hata katika suala zima la elimu. Tumekuwa na wataalamu wengi sana ambao wame-graduate chuo kikuu, wengine ni maprofesa, lakini wapo, elimu yao yaani hatuoni inawasaidia vipi kuwakomboa na maisha, wanaishi maisha magumu sana, ni maprofesa wapo chuo kikuu. Utumiaji wa elimu yao unatumika vipi katika kuleta mabadiliko katika nchi hii? Lakini ni kwa sababu ya ubora wa elimu ambayo wamekuwa wakiipata. Kwa hiyo mimi nafikiri ipo haja ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na walimu ambao wanasifa na uzoefu wa kutosha. Badala tu ya kumchukua mwanafunzi aliyemaliza kidato cha sita kwa sababu tu amesoma mpaka kidato cha sita ukasema elimu yake hii inamtosha kwenda kumfundisha mtu mwingine, na wakati mwingine amechagua kwenda kufanya teaching, amechagua kwenda kufundisha kwa sababu performance yake haikuwa nzuri. Sasa sioni maana yake kwamba ameshindwa kufanya vizuri katika masomo yake, halafu yeye umchukue aende akam-train mwingine. Kwa hiyo mimi naona iko haja ya kuachana na hii *crush program*, kwa sababu effect yake inaweza isionekane sasa hivi, yaani athari zake zinaweza zisionekane sasa hivi, lakini baada ya kipindi kirefu, kizazi hiki ambacho kinafundishwa na walimu hawa amabao ni *crush program*, *effects* zake, yaani athari zake ndio zitaonekana kule. Kwa hiyo naona iko haja ya msingi kabisa, ya kwamba tuwekeze, walimu wetu, tuwalipe walimu wetu mishahara mizuri, na walimu wawe ni wale watu ambao wana uzoefu wa kutosha, *performance* yao katika mambo ya kitaaluma imekuwa ni ya juu, na wakapelekwa chuoni, wakafundishwa vizuri, wakapewa *methodology* kwa ajili ya kufundisha. Mimi nafikiri kwa kufanya hivyo, tunaweza tukaenda mbali.

English translation:

Nicholaus: Another topic I have been thinking about is that the government has built many schools. The villages also have built many schools. The problem is that there is a high demand of teachers for those schools. What happens nowadays is that, if you have completed high school and you didn't get a chance to go to college, you can choose to teach for one or two years. Do you think this strategy will increase the standard of education? As you can see, students are in these schools, but there are not enough teachers. The government has decided to use those who have completed high schools to be teachers. What do you think?

Presenter: Yes! In my view, concerning those teachers from the "crash" programs, if you want to succeed, you must invest in education. And you cannot just invest in education, but you also need to consider at what level of education you are investing in. The problem here is that we view careers in education as a profession which doesn't need much experience. You don't need to be that intelligent. Sometimes, people view the field of education as the last career alternative. Those who didn't succeed in life are the ones who become teachers.

That has caused us to fall behind in educational matters. We have many professionals; some are professors who graduated from the University of Dar Es Salaam. However we don't see how they benefit from the education they have. They live poor lives. How is their education used to make changes in this country? It is because of the poor education they have. We need to have good teachers who have better education and enough experience, instead of accepting high school students as teachers, just because they have graduated from high school. It is not enough for them to be graduated from high school to become teachers. They cannot teach other students by using their high school knowledge. Some choose to go into teaching because their performance is poor. So how can it happen that if you fail in your studies, you can train another person? So I disagree with this crash program because the effects of this program may not be seen right now, but it will emerge some time in the future. The effects of the crash program will be seen by this generation who are being taught by these crash program teachers. It is good to invest in education. Our teachers should get a good salary, and they should be the ones who perform better academically. Those who attended teachers' college and those who have good teaching methodology are the ones who should become teachers. I think, by doing so, we will succeed.

About CultureTalk: CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated